# CLASS 7 END TERM 1 AUGUST 2021 KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

Mwaka ____1_____ tulipokuwa katika darasa la sita, tulipata nafasi ya kujifunza mambo ____2____. Daima, mwalimu wetu mcheshi ____3____ kwa vichekesho kila mara alipokuwa darasani. Tulielezwa msamiati wa vikembe kama vile ____4____ na msamiati wa maneno yenye maana zaidi ya moja, yaani ____5____, kwa mfano ____6____. Katika darasa hili, tutazidi kujifunza lugha kwa bidii ya ____7____. Elimu haina mwisho, ____8____.

1. A. jana B. huu C. juzi D. yenyewe
2. A. mingi mpya B. mengi mageni C. nyingi nzuri D. mwingi mwema
3. A. alituonea wivu B. alituvulia kofia C. alitushika mkono D. alituvunja mbavu
4. A. zumari, njuga na kipenga B. sime, singe na kifaru C. kimatu, buu na kitungule D. chawa, funza na kiroboto
5. A. vitenzi B. vitawe C. visawe D. vitate
6. A. gaga na kaka B. anika na anua C. runinga na televisheni D. chuma na kaa
7. A. kipepeo B. mende C. mchwa D. nzi
8. A. elimu ni bahari B. kawia ufike C. ushikwapo shikamana D. polepole ndio mwendo

Ni jambo la ____9____ sana kusikia visa vya watoto kutekwa nyara, kutendewa unyama na hata ____10____ mikononi mwa ____11____. Katika siku za hivi karibuni, zaidi ya watoto ____12____ walilipotiwa kutoweka. Cha kutia moyo ni kuwa ____13____ wengine tayari wametiwa ____14____ na huenda wakawasaidia maafisa wa ____15____ kufanya uchunguzi zaidi.

9. A. kuchangamsha B. kusikitisha C. kusikitika D. kufurahisha
10. A. kuuawa B. kuuliwa C. kuua D. kuwaua
11. A. majangili B. wafadhili C. wachungaji D. wakatili
12. A. ishirini na tano B. kumi na moja C. ishirini na wasita D. kumi na wanane
13. A. wauaji B. wafungwa C. washukiwa D. washirika
14. A. mbioni B. nguvuni C. jela D. polisi
15. A. afya B. trafiki C. polisi D. jeshi

***Kutoka nambari 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Kutokana na nomino maandishi, kitenzi ni
    A. mwandishi
    B. mwandiko
    C. andika
    D. waandishi

17. Chagua jina lililo tofauti na yale mengine.
    A. Mdalasini B. Bizari
    C. Kitunguu D. Pilau

18. Ni sentensi gani iliyo na **karibu** ya idadi?
    A. Shule ziko karibu kufungwa.
    B. Nina karibu rula tano.
    C. Usicheze karibu na barabara.
    D. Karibu mlevi agongwe na gari.

19. Chagua sentensi yenye istiara.
    A. Kaka ni mrefu kama mlingoti.
    B. Lo! Umemwua nyoka!
    C. Chakula hiki ni pilipili.
    D. Leo ni leo, msema kesho ni mwongo.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

20. "Ki" ya masharti inapatikana katika sentensi gani?
A. Nyanya akija atatuletea mihogo.
B. Kitoto kidogo kimejilaza chini.
C. Askari yule anatembea kishujaa.
D. Kikapu kimeanguka sakafuni.

21. Ni sentensi ipi iliyotumia kivumishi cha pekee kwa usahihi?
A. Tutaona wakati yoyote.
B. Tunda yoyote itamfaa mgonjwa.
C. Kucheka kwingine huudhi.
D. Shingo lote limefura.

22. Tambua sentensi yenye mnyambuliko sahihi wa vitenzi katika kauli ya kutendeka.
A. Mbwa wa Kasim hupenda kubweka.
B. Viazi vimepikwa vikapikika.
C. Wanafunzi wamelifagia darasa lao.
D. Bi. kizee anatembea polepole.

23. Kanusha sentensi ifuatayo:
**Kuimba kwake kulituvutia.**
A. Kuimba kwake hakukutuvutia.
B. Kuimba kwake hakutuvutii.
C. Kutoimba kwake kulituvutia.
D. Kutoimba kwake hakukutuvutia.

24. Tegua kitendawili hiki:
**Ninacho lakini sikioni.**
A. Jina B. Kisogo
C. Macho D. Ulimi

25. Ni sentensi gani iliyoakifishwa vilivyo?
A. Kumbe leo ni alhamisi!
B. Kimbieni mje, "Mwalimu akawaita."
C. Sasa ni saa saba kamili.
D. Ugonjwa wa Korona ni hatari, tusipojihadhari!

26. Ripoti kauli hii kwa usahihi.
Baba alimwambia Rosa, "Nitakuletea zawadi."
A. Baba alimwambia Rosa kuwa angempelekea zawadi.
B. Baba alimwambia Rosa kuwa nitakuletea zawadi.
C. Rosa aliambiwa kuwa angeletewa zawadi.
D. Rosa aliambiwa na baba kuwa atapelekewa zawadi.

27. Ni kiungo gani cha mwili kilicho tofauti na vingine?
A. Figo B. Kibofu
C. Mbavu D. Kisugudi

28. **Kufuli langu limepotea**, katika hali ya wingi ni
A. makufuli yetu yamepotea.
B. kufuli letu limepotea.
C. makufuli yangu yamepotea.
D. kufuli yetu yamepotea.

29. Nomino ***umbo***, ***yai*** na ***jani*** ni za ngeli gani?
A. I - ZI B. LI - YA
C. U - ZI D. I - I

30. Ni chombo kipi hapa husafiri huu ya reli?
A. Tuktuk B. Pikipiki
C. Kiberenge D. Matwana

***<u>Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu swali la 31 hadi 40.</u>***

Ulikuwa mwendo wa adhuhuri yapata kama saa tisa kasorobo hivi. Wengi wetu walilemewa na usingizi wakawa hawajiwezi kwa kugoteatea juu ya viti vyao. Chini ya mwembe huo kulikuwa na afueni kwelikweli. Upepo ulivuma kwa maringo huku miti mingine ikisujudu kwa heshima. Licha ya baadhi yetu kusinzia kutokana na shibe, wapo walioruka huku na kule kwa usumbufu, Naam, ni kawaida kila darasa kuwa hivi mwalimu asipokuwa kwani **<u>paka akiondoka, panya hutawala</u>**. Hata hivyo, kulikuwako kundi dogo lililoendeleza majadiliano kuhusiana na masomo mbalimbali.

Juhudi za kiongozi wetu kutuliza fujo ziliambulia patupu, zikawa sawa na kumpiga chura teke, ambapo ni kumsogeza mbele. Hatimaye, **<u>naye alibwaga silaha</u>** na kuamua kujiunga na lile kundi la majadiliano. Wanne hao pamoja na kiranja walijitenga nasi madomokaya kwa minajili ya kujaribu kuorodhesha baadhi ya nomino katika ngeli zao mwafaka. Hii ilikuwa kazi ya kila mmoja (kulingana na maagizo ya mwalimu) ila tuliamua kuchukua fursa hiyo "kupumzika."

Tangu asubuhi, hakuna mwalimu aliyetia guu. Wengi wao, kama si wote, hawakuzoea kutoa mafunzo chini ya mti badala ya darasani. Hata hivyo, si mara moja au mbili mwalimu mkuu aliturushiarushia macho ili kuhakikisha kulikuwako hali ya utulivu na labda, kubaini walimu gani walioweza kujitwika mzigo wa kutoa huduma hata katika mazingira magumu. Kila tulipomwona akiutazama upande wetu, tulitulia utadhani maji ya kina kirefu. Acha aondoe macho kwetu!

Mwishowe, aliamua kuja kutujulia hali.Mkononi alikuwa na buku jeusi lenye jalada gumu, kalamu kaibana baina ya kidole gumba na cha shahada. Alikuwa mwanamke njorinjori hivi mwenye shungi jekundu la nywele, tabasamu yake kaificha nyuma ya miwani yenye vioo vinene - miwani ambayo daima iliketi juu ya pua badala ya machoni.

"Hamjambo mabingwa?" Alitusalimu huku akiyasawazisha makalio yake juu ya kiti regerege cha mbao kilichokuwa mbele ya ubao wa kufutia machozi. "Kwa kuwa leo ni siku ya mwisho ya wiki hii, Jumatatu mtalipata darasa lenu limekarabatiwa kwani wazazi wenu walishatuma pesa za kujengea."

---

**31.** Kulingana na paragrafu ya kwanza, baadhi ya wanafunzi walisinzia kwa kuwa
A. walikuwa wachovu.
B. mwalimu hakuwa darasani.
C. walikuwa wameshiba mno.
D. hawakutaka kupiga kelele.

**32.** Ni vikundi vingapi vya wanafunzi vimejitokeza katika ufahamu?
A. Vinne B. Viwili
C. Vitano D. Vitatu

**33** Kwa kuwa '**<u>paka akiondoka, panya hutawala</u>**', neno **paka** hapa linarejelea
A. kiranja
B. mwalimu
C. hedimasta
D. mwandishi

**34.** Lile kundi la majadiliano lilikuwa na wanafunzi wangapi?
A. Watano B. Sita
C. Wanne D. Watatu

**35.** Kidokezi '**<u>naye alibwaga silaha</u>**' kinamaanisha
A. mwandishi alizidisha kelele.
B. kiranja alichoka.
C. majadiliano yalichacha.
D. Hedimasta alikuja.

**36.** Mwandishi wa habari hii alikuwa miongoni mwa wale
A. waliosinzia
B. waliojadiliana
C. waliopiga kelele
D. waliolala

**37.** Ni kwa nini wanafunzi walikuwa chini ya mti?
A. Darasa lao lilikuwa limekarabatiwa.
B. Walitaka kupunga upepo mwanana.
C. Waliyafuata maagizo ya mwalimu.
D. Darasa lao lilikuwa limebomoka.

**38.** Ni kwa nini walimu hawakufunza?
A. Walikuwa na shughuli tofauti.
B. Hawakuwa wamezoea kufunzia hapo.
C. Walikuwa wakilikarabati darasa.
D. Walifuata maagizo ya mwalimu mkuu.

**39.** Chagua kauli ambayo **si** ya kweli kulingana na kifungu.
A. Darasani si wanafunzi wote huwa watulivu.
B. Hayo yote yalitendeka Ijumaa.
C. Wanafunzi walimheshimu kiranja wao.
D. Hedimasta aliwajali sana wanafunzi hawa.

**40.** Kwa maoni yako, baada ya maelezo ya mwalimu mkuu, wanafunzi walibaki katika hali ya
A. huzuni B. hasira
C. wasiwasi D. furaha

---

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.</u>***

Katika mwaka, huwa kuna misimu au majira mbalimbali. Misimu mingine huwa mifupi huku mingine ikiwa mirefu ajabu. Mara nyingi, misimu hii tofauti tofauti husababishwa na ile hali ya dunia kulizunguka jua. Huenda tusiamini kuwa hili hutendeka ila utafiti wa kisayansi umebainisha hivyo.

Kunao msimu wa vuli. Huu huwa msimu wa mvua ndogo ndogo, rasharasha au mvua ya muda mfupi. Wakati huu wa mchoo, shughuli za shambani huwapo kulingana na aina ya mimea ambayo wakulima hupanda. Kumbuka, mimea mingine huhitaji kiasi kidogo tu cha mvua huku mingine ikihitaji mvua nyingi. Wakati huu, baridi huwapo ingawa si nyingi. Si kawaida kwa msimu huu kukatiza shughuli nyingi za wananchi. Mifugo na hata baadhi ya wanyamapori hufurahi kwa kuwa nyasi na majani wayalayo huchanua na kukoza rangi ya kijani kibichi.

Mvua nyingi hushuhudiwa wakati wa masika. Huu huwa msimu wenye kuwatia wakulima wasiwasi mwingi kwa sababu huenda ukasababisha mafuriko au gharika. Mvua iwapo nyingi kupita kiasi katika msimu huu wa kifuku, madaraja husombwa, makao huharibiwa, binadamu na mifugo hupoteza maisha huku maradhi au magonjwa mbalimbali yakizuka. Magonjwa yawezayo kuibuka wakati huu ni kama vile kichocho, kipindupindu, kuendesha na homa ya matumbo, yaani taifodi.

Baridi shadidi hushuhudiwa katika majira ya kipupwe. Hapa baridi huwa kali kuliko wakati wa vuli. Mara nyingi utagundua kuwa watu huvalia mavazi mazito ili kuwakinga dhidi ya magonjwa kama vile kichomi au nimonia. Wengi hususia shughuli za alfajiri na mapema wakihofia kukumbana na baridi inayopenya hadi mifupani.

Balaa huzuka wakati wa kiangazi ama chaka maana huu huwa msimu wa joto na jua kali bila hata tone la mvua. **<u>Mimea hukauka kaukau</u>** huku wanyamapori na wanyamahowa wakibaki fremu tu. Wakati huu, wakulima hulazimika kunyunyizia mimea yao maji kwani lisilobudi hubidi.

---

**41.** Chagua kauli iliyo ya kweli kulingana na aya ya kwanza.
A. Katika mwaka mzima, misimu huwa haifanani.
B. Wanasayansi wamebainisha tofauti za misimu.
C. Ni vigumu kuamini tofauti za urefu wa misimu.
D. Mvua ndogo ndogo hushuhudiwa wakati wa vuli.

**42.** Ni nini ambacho msemaji anasema huenda tusiamini?
A. Mabadiliko ya misimu.
B. Ile hali ya jua kuizunguka dunia.
C. Utafiti wa wanasayansi.
D. Ukweli kuhusu jua kuzungukwa na dunia.

**43.** Mwandishi ametaja majira mangapi?
A. Matatu
B. Manne
C. Mawili
D. Matano

**44.** Ni msimu upi haujalinganishwa na jina lake la pili?
A. Mchoo - Vuli
B. Masika - Kifuku
C. Kifuku - Gharika
D. Kiangazi - Chaka

**45.** Chagua misimu miwili ambapo baridi hushuhudiwa.
A. Vuli na kiangazi B. Kipupwe na vuli
C. Chaka na mchoo D. Masika na kiangazi

**46.** Kulingana na taarifa, ni ugonjwa gani hauwezi kuibuka wakati wa masika?
A. Nimonia B. Kipindupindu
C. Kichocho D. Taifodi

**47.** Wanyama hufurahi zaidi wakati wa
A. kiangazi B. vuli
C. masika D. kipupwe

**48.** Hatari ya kuugua kichomi huweza kuwa katika msimu upi?
A. Mchoo B. Chaka
C. Kifuku D. Kipupwe

**49.** Je, ni kwa nini balaa huzuka kulingana na aya ya mwisho?
A. Mimea hunyunyiziwa maji.
B. Wanyama hunona kupindukia.
C. Wanyama huwa na afya duni.
D. Nyasi na majani huchanua.

**50.** Kifungu **<u>mimea hukauka kaukau</u>** kimetumia
A. istiara B. tanakali ya sauti
C. nahau D. tashbihi